# Pambazuko

Toleo Namba 145 | Jumatatu, Oktoba 27-Novemba 2,2025

# Ni wakati wa uamuzi

- Kete sita za ushindi CCM uchaguzi mkuu

Uk. 6&7




Rais Samia Suluhu Hassan

## Udasa yashauri dawa ya utekaji, UDSM yajitenga

JUMUIA ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Udasa), imeshauri vyombo vya usalama kuchunguza kwa uwazi na kwa haraka matukio yote ya watu kupotea na wengine kudaiwa kutekwa. Uk. 9



## Wafurahia kifungo cha waliotaka kumteka Tarimo

"SASA tumeona haki imetendeka, hili ni jambo zuri sana na hongera kwa vyombo vya serikali kwa kulivalia njuga suala hili hadi mwisho wake." Uk. 12

## Wahariri wahimiza amani, mwingine akomalia haki

Uk. 14&15

# Tahariri/Katuni

## Tukapige kura kwa busara, amani itawale

KESHOKUTWA - Jumatano ya Oktoba 29 mwaka huu, Watanzania wenye sifa na waliojiandikisha watapata fursa ya kupiga kura kuchagua viongozi watakaokuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Waliojiandikisha watakuwa na haki ya kupiga kura kumchagua rais, mbunge pamoja na diwani, na kwa upande wa Zanzibar, watachagua pia wawakilishi.

Kama ilivyo kawaida kampeni za uchaguzi, ambazo zinakamilika kesho, zilitawaliwa na hoja kutoka kwa vyama na wagombea vikieleza nini wamepanga kuwafanyia Watanzania iwapo watachaguliwa.

Sisi katika Pambazuko tunaamini kuwa wapiga kura wamewasikiliza na kuwaelewa wagombea wote na sasa kazi iliyobaki ni kwao kufanya uamuzi.

Hiyo Jumatano, wenye sifa na utayari watasogea kwenye vituo vya kupigia kura na kuamua nani wanamchagua kuwaongoza; iwe kwenye urais, ubunge, udiwani na uwakilishi.

Timu ya Pambazuko ambayo inajumuisha viongozi wa taasisi inayosimamia, wahariri, waandishi, na watendaji wengine, tunawaombea wote watakaokwenda kupiga kura kufanya hivyo kwa busara itakayoiwezesha nchi kupata viongozi makini ambao wataisogeza mbele katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kila anayekwenda kupiga kura anatakiwa kukumbuka kuwa anayemchagua ndiye atakayebeba dhima ya kuletea maendeleo.

Iwapo utakosea na kumchagua mtu asiyefaa, utalazimika kuishi naye kwa kipindi hicho chote na hautakuwa na wa kumlaumu isipokuwa wewe mwenyewe.

Katika kipindi hiki cha kampeni pia tumeshuhudia kupanda kwa joto la kisiasa kutokana na kuibuka kwa kundi la watu waliohamasisha kufanyika kwa maandamano siku ya uchaguzi.

Tulishatoa maoni yetu kuhusiana na hilo tukisema kuwa tunaheshimu haki ya watu hao kuandamana, lakini kwa kuwa siku waliyopanga kuandamana ilikuwa imeshapangiwa tukio jingine kubwa na muhimu kwa nchi, hivyo basi, tumekuwa tukihimiza kwamba wangetafuta siku nyingine ya kutekeleza azma yao ili kutoa uhuru kwa wale watakaopiga kura kufanya hivyo kwa utulivu na amani bila tishio la aina yoyote.


Tunaamini kuwa Watanzania wamekuwa wakitusikia na kuamini kuwa wataekeleza jambo kubwa la siku hiyo ili kujiwekea mustakabali kwao na watoto, wajukuu, vitukuu na hata vilembwe.

Pambazuko tunatamani kuona kukitamalaki amani na utulivu siku hiyo ya Jumatano – Oktoba 29 ili kuwapa wapiga kura fursa nzuri zaidi ya kufanya uamuzi.

Kila heri kwa wote wanaokwenda kupiga kura kuchagua viongozi na wasiopenda kutumia haki yao hiyo ya kikatiba, wasiwe chanzo cha vurugu na kuleta rabsha kwa wengine.

Amani na haki kwa Mama Tanzania iwe nia ya kwanza na mambo mengine yafuate baadaye.

## Katuni





*Mwonekano wa mabanda ya wafanyabiashara yaliyopo kwenye hifadhi za barabara yanayosababisha kero kwa watembea kwa miguu katika eneo la Mbezi jijini Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu).*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

## WASILIANA NA CHUMBA CHA HABARI; 0784 211 716

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na pale

## Hali bado tete Cameroon

WAKATI Tume ya Taifa ya Uchaguzi nchini Cameroon ikiendelea na mchakato wa kupata idadi kamili ya kura za mshindi wa kiti cha urais, vyombo vya usalama vinaendelea kukamata na kufungulia mashtaka "vijana watukutu."

Bado kuna maandamano katika miji mikubwa ikiwamo, mji wa kaskazini wa Garoua, ambao ni ngome ya mpinzani, Issa Tchiroma Bakary ambaye tayari amejitangaza kuwa mshindi wa kiti cha urais. Hata hivyo, matokeo rasmi bado hayajatangazwa, huku Rais Paul Biya akishutumu upinzani kujitangazia ushindi.

Kutokana na "sintofahamu" ya matokeo, kuna uwezekano mkubwa wa kuibuka kwa vurugu baada ya kutangazwa bila kujali upande gani utashinda. Ikiwa upinzani utaibuka kidedea, chama tawala kitapinga na kinyume chake. Hapo ndipo inatarajiwa kulipuka kwa vurugu.

Mwishoni mwa wiki iliyopita - Oktoba 22, 2025, Waziri wa Mambo ya Ndani, Paul Atanga Nji alisema "wasumbufu" waliokamatwa walitumwa na wachochezi kutoka ndani na nje ya nchi, hivyo lazima washughulikiwe.



## Kenyatta na mkewe vipi?

WAKENYA wameendelea kujiuliza kinachoendelea kati ya rais mstaafu, Uhuru Kenyatta na mkewe, Magret Gakuo Kenyatta, baada ya kutoonekana kuongozana na mumewe kwenye maziko ya Raila Odinga.

Katika mazishi hayo yaliyofanyika eneo la familia ya Odinga, huko Bondo, Uhuru alionekana akiwa peke yake bila mkewe, hivyo kuzidisha uvumi kuwa wawili hao wameachana.

Hata hivyo, uvumi huo haujathibitishwa rasmi, pamoja na kwamba umeendelea kushika kasi, baada ya Uhuru kuondoka madarakani mwaka 2022.



## Jacob Zuma kufilisiwa

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, bado anakabiliwa na majanga kutokana na matumizi mabaya ya dhamana aliyopewa kuongoza taifa hilo tajiri Afrika.

Baada ya kulipa fedha nyingi kwa kupatikana na hatia ya kutumia fedha za walipa kodi kujenga jumba lake la kifahari, sasa anatakiwa kulipa kiasi cha shilingi bilioni 4.12 (Rand milioni 29) kwa kubainika kutumia kiasi hicho kulipa mawakili kwenye kesi aliyoshtakiwa binafsi akiwa rais.

Mahakama imempa siku 60 kukamilisha malipo ya fedha hizo kwa kulipa kupitia hazina ya nchi hiyo. Endapo atashindwa, korti hiyo ya juu imeamuru mali zake; zinazohamishika na zisizoweza, kuunganishwa na kupigwa mnada ili kutumika kumaliza deni hilo.

Jaji Anthony Millar huyo wa Mahakama Kuu ya Gauteng, Masjala ya Pretoria, imetamka pia, rais huyo wa zamani aliyekumbwa na kashfa akiwa madarakani, kulipa na riba, huku akitaka pensheni ya Zuma kuunganishwa pia.

## Makamanda Mali watimuliwa

RAIS wa mpito wa Mali amewafuta kazi makamanda watatu waandamizi wa jeshi, baada ya kuwashutumu kuwa wamekuwa na "utendaji mbaya kwenye majukumu yao."

Rais Assimi Goita aliwaachisha kazi wafuatao; naibu kamanda wa jeshi, mkuu wa usalama jeshini na mkuu wa kikosi cha ardhini.

Tangu 2012, Mali imekuwa na matatizo ya kiusalama kutokana na mashambulizi ya magaidi wenye uhusiano na makundi ya Al Qaeda na Daesh. Rais Goita aliingia madarakani kufuatia mapinduzi ya kijeshi ya 2020 na 2021 akiahidi kuimarisha usalama.

Na Mzee TAI

Jicho la Tai

# Tuhimizane kupiga kura Jumatano

KESHOKUTWA, yaani Jumatano ya Oktoba 29, Tanzania inaenda kuandika historia nyingine ya kufanya uchaguzi wake wa saba tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi.

Ni historia ambayo hutokea kila baada ya miaka mitano, ambapo wananchi wenye sifa, hutumia uhuru wao wa kikatiba kuchagua viongozi wanaowataka; kuanzia rais, wabunge, madiwani, lakini pia – kwa upande wa Zanzibar, kuwapata wawakilishi wao.

Viongozo wote hawa watapatikana kwa kupiga kura, kura kuhesabiwa na kutangazwa matokeo na wahusika waliopewa kandarasi ya kufanya kazi hiyo muhimu kwa mustakabali wa Tanzania na watu wake.

Mwezi mmoja na ushei uliopita, wagombea wa nafasi hizo wamekuwa wakijipitisha kwa wananchi kunadi sera zao na kutangaza ilani za vyama vyao, kwamba wamepanga kuwafanyia nini Watanzania kwa kipindi cha miaka mitano, watakapokuwa wamepewa dhamana ya kuongoza.

Ni katika kipindi hicho cha kampeni, tumewasikia wanaowania kuingia, kuishi na kutumika wakiwa ndani ya nyumba namba moja Tanzania; Ikulu. Tuna bahati siku hizi ikulu zipo nyingi, lakini kubwa na zinazofahamika zaidi ni mbili; Dar es Salaam na Dodoma. Lakini, ipo ya tatu ambayo mgombea anayeshinda huamua iwe wapi; nyumbani kwao, kwa wake zake au hata eneo analopenda kuwa.

Tangu kuanza kwa kampeni, mambo yamekuwa mengi sana. Kila nikipata nafasi, nimekuwa nikihudhuria mikutano ya wagombea, hasa wa urais. Huku nimekuwa nikiandika ahadi zao ili nije kuwabana, mmoja wao anapokuwa ameshinda.

Nimemsikiliza mgombea wa CCM, nikawasikiliza wale wengine wa vyama vya upinzani; Chaumma, CUF, Tadea, AFFP, UDP na vingine.

Katika kuchambua, nikabaini nani anashinda kwa kuwa wagombea wengi wa nafasi hiyo kuu ya kuajiriwa na Watanzania, wanapwaya na wamekuwa wakibwabwaja tu bila kuonekana kuwa makini.




Yaani mgombea mmoja anatamka waziwazi kwamba yeye hana uwezo na akishinda ataiacha kazi hiyo kwa mgombea mwenye uzoefu. Najiuliza, huyu anagombea ili iweje. Mwingine badala ya kueleza ataifanyia nini Tanzania na watu wake - kwa maana ya kuleta maendeleo, yeye anasema akiingia Ikulu, kitu cha kwanza ni kupiga marufuku vitanda vya sita-kwa-sita, maana anataka wenzi wazaliane zaidi. Nani kamwambia huyo kila wanaooana wanataka kupata watoto?

Hata hivyo, nikampenda zaidi mgombea mmoja, huyu yeye kila akitangaza jambo moja, anapiga muziki na kualika mashabiki wake wacheze. Mambo ya ilani siyo shida zake kabisa. Shida ya nini wakati serikali imempa "viet" – tena kilomita zero, na ana mlinzi na dereva, hata kama hana pesa za kuongeza mafuta.

Sasa kibaya zaidi nilichokiona ni baadhi ya wajukuu zangu eti wananifuata na kuniuliza endapo nitapiga kura kweli. Nawaambia nitapiga kura na kuwa mtu wa kwanza kwenye mstari hiyo keshokutwa.

Kwanini nisipige kura, kuna nini kibaya kutumia haki yangu kuchagua viongozi wangu. Na nimewahimiza wote siku hiyo kuongozana nami, atakayekaidi atakiona cha moto. Kwanini wasipige kura wakati wana sifa zote. Kuacha kwao kutumia haki yao ya kikatiba ndiyo mwanzo wa kutupatia viongozi wabovu.

Nami nahimiza Watanzania wote twendeni tukapige kura hiyo Jumatano – Oktoba 29, 2025.

# Ni wakati wa uamuzi



*Rais Samia Suluhu Hassan*

Na Mwandishi WETU

BAADA ya miezi miwili ya kampeni ambayo wanasiasa waliokuwa wanatamba majukwaani, wakitoa ahadi lukuki kwa wananchi, sasa umefika wakati wa wao kunyamaza.

Umefika wakati wa wananchi nao kuzungumza, siyo kwa maneno tena, bali kwa kalamu na tiki.

Keshokutwa – Jumatano Oktoba 29, Watanzania walioandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapiga kura, watapata haki yao ya kuamua nani awe rais wao, mbunge wao, diwani wao au mwakilishi wao.

Siku hiyo itakapofika, kwa kufuata utaratibu uliopo kisheria, wanasiasa hawana nguvu tena ya kuwaelekeza wananchi ni nini cha kufanya, kwani kila mtu atafanya uamuzi kulingana na utashi wake.

Kama kuna mwanasiasa ambaye ameshindwa kumshawishi mwananchi kwa hoja – hadi kesho, basi wakati huo umeshapita na sasa ni zamu ya wananchi kuamua.

Jumla ya vyama 17 vimesimamisha wagombea urais, wabunge na madiwani.

Vyama vinavyoonekana kuwa na upinzani ni chama tawala; Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Ukombozi wa Umma (Chaumma) na Chama cha ACT Wazalendo chenye ushawishi mkubwa Zanzibar.

Pamoja na mchuano miongoni mwa wagombea, bado mshindi hadi sasa hajajulikana ingawa kila chama kilichosimamisha wagombea, kimekuwa kikijigamba, kwamba kitaibuka mshindi.

CCM wanasema watashinda kwa kishindo katika nafasi ya urais ambako mgombea wao Samia Suluhu Hassan, anatetea nafasi yake.

Aidha, CCM imejinasibu kuibuka na idadi kubwa ya kura, na kwamba kitapata wabunge na madiwani wengi zaidi.

Chaumma nao wanasema watashinda na wanawatoa hofu wafuasi wao, kwamba mgombea urais wao, Salum Mwalimu, atapata kura nyingi kukiwezesha chama hicho kuunda serikali.

Licha ya kutokuwa na mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, ACT Wazalendo wanajigamba kuwa kitashinda katika majimbo mengi na kukiwezesha kulikamata Bunge.

Lakini, chama hicho kinajipigia upatu kushinda urais wa Zanzibar ambako mgombea wake, Othman Masoud Othman, maarufu kama OMO, atamshinda Mgombea wa CCM, Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Pamoja na hali hii ya vyama na wagombea kujimwambafai, upo ukweli unaotokana na mambo halisi yalivyo katika uwanja wa mapambano.

Tathmini iliyofanywa kwa muda sasa na Pambazuko imetoa mwelekeo unaoonyesha kuwa, CCM kina nafasi kubwa ya kuibuka na ushindi katika nafasi zote kwa maana ya urais, ubunge, udiwani na uwakilishi.

Inaendelea Uk. 7

# Ni wakati wa uamuzi

Inatoka Uk. 6

**Aina ya mgombea urais**

Yapo mambo kadhaa ambayo Pambazuko imeyazingatia katika uchambuzi wake na kufikia hitimisho hilo.

Mgombea wa chama hicho ambaye ni rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan, amebeba mengi yenye faida kwa chama hicho.

Yeye ni kete kubwa hasa ukizingatia kuwa anatetea kiti hicho.

Katika kampeni yeye ni mgombea pekee ambaye ameweza kuwaeleza wananchi kile ambacho chama chake kimefanya.

Wengine hawana nafasi hiyo kwa sababu hawakuwa katika nafasi ya utekelezaji na hawakuwa madarakani.

Rais Samia amekuwa madarakani kwa zaidi ya miaka minne tangu alipofariki mtangulizi wake, Rais John Magufuli.

Kwa ufupi, Rais Samia na CCM, wana kitu cha kuonyesha kwa Watanzania wakati wakiomba kuaminiwa tena, tofauti na vyama vingine ambavyo havina cha kuonyesha.

**CCM na vyombo vya habari**

Jambo jingine ambalo linaibeba CCM ni jinsi ambavyo chama hicho kimekuwa kinara kwenye vyombo vya habari.

Ukiacha nafasi ya kuandikwa au kujitangaza kupitia matangazo, ukubwa wake, wingi wa wagombea na aina ya hoja wanazotoa wagombea wake majukwaani, vimevifanya vyombo vingi vya habari nchini kulazimika kuandika au kutangaza kuhusu CCM kuliko chama kingine chochote.

CCM na wagombea wao wanatangazwa kila mahali, wanatangazwa katika televisheni zote, wanatangazwa katika vituo vya redio na pia wanajinadi kwa nguvu na habari zao kutangazwa katika mitandao mingi ya kijamii na mabango ya picha zao zimesambaa katika maeneo mbalimbali nchini.

Licha ya kutegemea vyombo vya habari binafsi kwa ajili ya kujitangaza, Rais Samia na CCM kwa ujumla wake, wanatumia vyombo vya habari vinavyomilikiwa na chama chao vikiwamo Radio Uhuru, Channel Ten, magazeti ya Uhuru na Mzalendo na magazeti yale yanayoendeshwa na taasisi zake.

Vyombo hivyo vya habari ni kete nyingine muhimu iliyokibeba chama hicho na hivyo kukifanya kiendelee kujulikana na kujiimarisha zaidi katika kampeni tofauti na vyama vya upinzani.

Taarifa za wagombea wa CCM ziliwafikia wananchi wengi ukilinganisha na vyama na wagombea wengine.

**Msuli wa kifedha**

CCM ina ukwasi wa kutosha. Hiyo imekiwezesha chama hicho kufanya kampeni kwa ufanisi mkubwa na kuyafikia maeneo mengi nchini ukilinganisha na wagombea wengine ambao walikwama kwenye kampeni zao kutokana na ukosefu wa fedha.

Wapo wagombea wengi wa upinzani ambao safari hii wameweza kuzunguka maeneo mengi kidogo kutokana na kupewa magari na Tume Huru ya Uchaguzi (INEC).

Kama isingekuwa uamuzi wa INEC, kuna wagombea ambao wala wasingeweza kwenda zaidi ya mikoa mitatu kufanya kampeni.

Mwanzoni mwa Agosti mwaka huu, CCM kiliitisha harambee ya kutafuta fedha kwa ajili ya uchaguzi mkuu ambapo kilifanikiwa kupata shilingi bilioni 86.31 kati ya shilingi bilioni 100 zilizokuwa zimepangwa.

CCM pia kina marafiki wa ndani wakiwamo wafanyabiashara wenye uwezo mkubwa kifedha ambao mara kadhaa wamekuwa wakikisaidia chama hicho kwa hali na mali.

Pia, kina miradi mingi inayoingiza fedha na pia kina urafiki na vyama vingine vya kisiasa nje ya nchi ambavyo navyo vimekuwa vikikiunga mkono katika mazingira tofauti tofauti.

Inaendelea Uk. 8






# Ni wakati wa uamuzi

Inatoka Uk. 7

Kwa maana hiyo, CCM kina uwezo wa kujitangaza popote, kwa gharama zozote, kwa njia tofauti tofauti iwe ni kwa kubandika barabarani matangazo ya wagombea.

Pia, chama hicho kina uwezo wa kutumia helkopta kuzunguka maeneo mengi kwa muda mfupi, hivyo kuwafikia wananchi kwa urahisi.

**Mtandao nchi nzima**

Jambo kubwa ambalo limekibeba CCM ni mtandao wake uliosambaa nchi nzima.

Umri wake mkubwa umekiwezesha chama hicho kufika katika kila pembe ya nchi wakati kuna baadhi ya vyama vya siasa ambavyo havitambuliki nje ya miji mikubwa ingawa navyo vinataka kushika dola.

Mtandao huo unakiwezesha CCM, kuratibu shughuli zake zikiwamo kampeni kwa urahisi.

Tangu chama hicho kilipoanzishwa Februari 2, mwaka 1977, kimefanikiwa kujiimarisha na kuwa na wanachama wengi zaidi kuliko chama kingine cha siasa nchini. Kinajitangaza kuwa na zaidi ya wanachama milioni 12.

Kutokana na mtanado huo, CCM kimefanikiwa kusimamisha wagombea wa udiwani katika kata zote nchini, kimesimamisha wagombea ubunge na uwakilishi katika majimbo yote nchini.

Wagombea hawa wa ngazi zingine, ni fursa kwa mgombea wao wa urais kufikia watu wengi hata kama hayupo eneo hilo.

**Ukongwe, uzoefu katika chaguzi**

CCM ni moja ya vyama vikongwe vya siasa Afrika, kwa hiyo, kina uzoefu wa kutosha wa kushiriki uchaguzi wowote wa kisiasa bila kujali ukubwa au udogo wa vyama vya upinzani kinavyoshindana navyo.

Chama hicho kina mbinu nyingi za kukifanya kishinde, kinaweza kuazima mbinu za ushindi kutoka vyama rafiki, kinajua namna ya kukaa na wapiga kura nchi nzima.

Chama hicho kinao wanasiasa waliobobea katika siasa, kina wataalam wazuri wa propaganda, kina wanachama wanaojua kujenga hoja majukwaani.

Kwa hivyo, siyo ajabu kuwa, CCM kinaaminika zaidi miongoni mwa wananchi.

Vyama vya upinzani havina fedha za kutosha, havina umaarufu wa kutosha, baadhi ya wagombea wao hawajulikani na pia vyama hivyo havina wafuasi nchi nzima watakaovisaidia kupata ushindi katika uchaguzi mkuu.

Kukosa upinzani wa nguvu

Kutoshiriki kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) katika uchaguzi wa mwaka huu, umekipa mwanya CCM kukabiliana na upinzani dhaifu, hivyo kuwa na ushindi wa uhakika.

Chadema hakikushiriki uchaguzi huo kwani kinaamini kuwa siyo huru na wa haki.

Kwa muda sasa, chama hicho kimekuwa kikishinikiza mabadiliko ya sheria za uchaguzi kwa lengo la kuweka mazingira ya usawa katika uchaguzi na harakati za kidemokrasia nchini.

Kwa upande mwingine, ACT Wazalendo, ambacho kilipanga kumsimamisha mmoja wa wakosoaji wakubwa wa serikali, Luhaga Mpina, kimejikuta nacho kikienda kwenye uchaguzi bila mgombea urais baada ya Mpina kuenguliwa.

Baadhi walidhani Chaumma, ambacho kimejizolea umaarufu katika siku chache kuelekea uchaguzi mkuu, kingeweza kuleta upinzani mkubwa kwa CCM, lakini hali ya mambo inaonyesha chama hicho hakikuleta ushindani kwa CCM

# Udasa yashauri dawa ya utekaji, UDSM yajitenga

**Na Mwandishi WETU**

JUMUIA ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Udasa), imeshauri vyombo vya usalama kuchunguza kwa uwazi na kwa haraka matukio yote ya watu kupotea na wengine kudaiwa kutekwa.

Udasa imetoa ushauri huo kupitia tamko lao lenye kurasa 11 lililosainiwa na mwenyekiti wake, Profesa Elgidius Ichumbaki na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii Oktoba 23,2025.

Pamoja na mambo mengine, tamko hilo lilieleza kuwa matukio ya aina hiyo yanatishia uhuru wa kujieleza na misingi ya haki za binadamu nchini. "Tunawategemea viongozi wetu wa kitaifa kuliokoa taifa na kuepuka kutoa kauli zinazotonesha majeraha ya kukandamizwa na kuonewa kwa kutumia dola na vyombo vingine vya usalama," imesema tamko hilo.

Vilevile jumuia hiyo imeshauri baada ya uchaguzi mkuu kupita, iindwe tume ya kijaji au kamati maalum ya Bunge ambayo nayo itachunguza matukio hayo.

"Tume hiyo ya kijaji au kamati ya bunge itabainisha kiini cha tatizo na kutoa mapendekezo ili hatua stahiki zichukuliwe kukomesha vitendo hivi..."

"Hata kama utekelezaji wa mapendekezo hayo utahitaji utashi wa kisiasa, ripoti ya tume hiyo itaweza kuwafariji waathiriwa wa matendo hayo".

Jumuia hiyo imetaka Bunge lijalo litambue kuwa lenyewe ni muhimili unaojitegemea na liko kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

"Bunge linapaswa kuwa na wivu mkuu juu ya hadhi na uhuru wake. Itafaa kama wabunge watatunga sheria ya kuwakinga raia dhidi ya nguvu za vyama wanapogombea nafasi mbalimbali za uongozi," imesema tamko hilo.

> **"Hata kama utekelezaji wa mapendekezo hayo utahitaji utashi wa kisiasa, ripoti ya tume hiyo itaweza kuwafariji waathiriwa wa matendo hayo".**

Kuhusu uchaguzi mkuu wa Oktoba 29,2025, Udasa imesema ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania mwenye sifa kushiriki kupiga kura.

Imezitaka pande zinazohusika na mivutano ya kisiasa kuelekea uchaguzi huo, kutambua makosa yaliyofanyika na kuchukua hatua stahiki kurekebisha hali hiyo.

**UDSM yajitenga na tamko hilo**

Muda mfupi baada ya Udasa kutoa tamko hilo, Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) umejitenga na tamko hilo.

Kupitia taarifa iliyotolewa Oktoba 23,2025 na Makamu Mkuu wa UDSM, Profesa William Anangisye, imeeleza kuwa haitambui tamko hilo wala kushiriki kwa namna yoyote katika kuandaa maudhui yake.

Taarifa hiyo imesisitiza kuwa Udasa ni jumuia huru inayojitegemea ndani ya chuo hicho na misimamo yake haiwakilishi misimamo ya chuo hicho.

"Chuo hiki kitaendelea kuwa taasisi ya umma inayozingatia misingi ya kitaaluma, Katiba na Sheria za nchi, pamoja na maadili ya umma. Tutaendelea kujihusisha na mijadala yenye tija kwa maendeleo endelevu na mshikamano wa kitaifa," imesema sehemu ya taarifa hiyo.

Kutokana na hilo, UDSM imetoa mwito kwa Watanzania wote wenye sifa za kisheria kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 29, 2025, kwa amani, utulivu na uzalendo, ikieleza kuwa amani ni msingi wa maendeleo, demokrasia, na ustawi wa taifa.

Mara kadhaa, Serikali ya Tanzania imekuwa ikikanusha kuhusika kwa namna yoyote na vitendo vya utekaji au watu kupotea.

Kwa upande wa Jeshi la Polisi ambalo limekuwa likishutumiwa, limekuwa likieleza kuwa kumekuwa na matukio ambapo baadhi ya watu waliodai kutekwa baadaye walithibitishwa kujiteka wenyewe na kuongeza kuwa linaendelea kufuatilia kila taarifa inayotolewa.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Tukumbushane bila kufokeana

NIMESEMA hii ni wiki ya kubembelezana siyo kutishana. Ukibembeleza unapata; ukitishia, mchumba anaingia mitini.

Nimebaini kuna watu wanahujumu wagombea na kufukuza wapiga kura. Wagombea shitukeni, mnahujumiwa!

Tutazame mifano michache. Kuna tabia sasa ya matumizi ya viongozi wa dini - mkitaka viongozi wa dini wasikilizwe na kuheshimiwa na waumini; basi serikali ndiyo ianze kuwaheshimu na kuzingatia maoni yao.

Wananchi wakiona serikali inaheshimu na kuzingatia ushauri wa viongozi wa dini, basi wananchi nao watawaheshimu viongozi wa dini kwa kile wanachoshauriwa.

Mara kadhaa sisi viongozi wa dini tunawaambia msinywe pombe, msizini, msitumie uzazi wa mpango- kwani mmeacha? Kwa nini? Kwa sababu serikali ndiyo ya kwanza kupuuza tunachowaambia waumini.

Hapa ninachokiona, kuna viongozi wa dini tulikuwa tunaheshimika kiasi fulani, lakini tumesukumizwa kwenye matope.

Heshima tuliyoijenga muda mrefu, inachafuliwa na hotuba ya dakika tano. Huu ni ukatili kwa viongozi wa dini na watu mashuhuri wanaosukumizwa bila utashi ili waseme wasichokiamini.

Kuhusu utawala wa sheria, njia nzuri, rahisi, nyepesi na ya gharama nafuu ya kusimamia utawala wa sheria, ni kwa serikali kuheshimu na kufuata utawala wa sheria.

Wananchi wakiona serikali inaheshimu sheria kuliko matamko, watafuata na kuheshimu sheria. Ukiona "Hebeas corpus" (kulazimisha waliofichwa mahabusu kuletwa mahakamani), zimepamba moto, ujue mtunga sheria anavunja sheria.

Miaka yote watu hukamatwa na kufunguliwa mashtaka hata ya uwongo. Hapakuwa na kuteka, kuficha, kukana, kusafirisha kwa kificho na kukanusha ukweli. Tubadilike, tutaona matokeo ndani ya muda mfupi.

Kuna hili jambo la matumizi ya polisi Siku ya Kupiga Kura, ambapo sasa wanaonekana polisi wengi na magari mengi mitaani siku ya kupiga

**Kinachowapa ajira machawa ni tofauti ya maoni. CCM ni nzuri kwa kuwa kuna Chaumma. Ikibaki peke yake, haitamaniki.**

kura, yana maana kuu mbili za haraka; kwanza ni kuwalazimisha watu kupiga kura, kuwazuia watu kupiga kura na najua ipo ya tatu ambayo iko vichwani mwa polisi, lakini haiaminiki na watu.

Mimi ni mtu, nawaambia yanayosemwa na watu.

Maandamano hayapo. Polisi ndio wataandamana. Ni vyema sasa polisi wakaondolewa mitaani. Kama kuna watakaoandamana, wasindikize bila kuwazuia wanaotaka "kutiki." Huo ni utawala wa sheria, siyo wa matamko. Uchaguzi utapita, sisi tutabaki.

Ni muda sasa wa kuacha kupigana na maoni.

Siku tukiamka asubuhi tukakuta watu wote wanatiki, wamevaa kijani, wanaimba "Bagonza Mitanoo Tena," wanasema katiba mpya ilaaniwe, hatutaki tume huru na tunataka chama kimoja tu; siku hiyo hata machawa watakimbia nchi.

Kinachowapa ajira machawa ni tofauti ya maoni. CCM ni nzuri kwa kuwa kuna Chaumma. Ikibaki peke yake, haitamaniki.

Tungeheshimu maoni tofauti, hata mwenye shahada ya kupiga kura iliyofutikafutika asingeruhusiwa kupiga kura.

Tunakoelekea hata asiyejiandikisha atapiga kura ili wawe wengi. Tuache kupigana na maoni ya watu, chaguzi zitaheshimika.

Dhambi ya makusudi ni kumkufuru Roho. Kutenda dhambi makusudi ukipanga kutubu baadaye, ni kufuru.

Mama mkwe akikuzingua, mzingue bintiye, hakika mtaheshimiana.

Turudi mezani; hatupotezi, tunapata.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Ninautafakari Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29

NINATAFAKARI sana hali ninayoiona na kuifuatilia hapa nchini kwa kipindi sasa.

Nikiiangalia nchi yetu ya Tanzania, nimekuwa na maswali mengi mno ambayo sijui ni nani anaweza kunisaidia kuyajibu.

Katika miaka ya nyuma, kipindi kama hiki tunapoelekea ukingoni kwenye uchaguzi mkuu, mijadala ilitawaliwa kuhusu yale yaliyosemwa na wagombea kwenye mikutano ya kampeni.

Lakini, mwaka huu mijadala ni kama imezimwa kutokana na hofu inayotokana na vitisho. Watu wanazungumzia maandamano na wengine wakipinga maandamano.

Mitandao ya kijamii imejaa mambo mengi – mengine ya kweli na mengine ya uongo.

Kuna wakati ungetegemea kusikia kutoka kwa mamlaka husika iwapo yasemwayo ni kweli au siyo kweli, lakini naona kuna hali ya ukungu kutoka wanaotegemea kusikia ukweli na wale wanaotegemewa kuutoa ukweli.

Mfano, tunasikia kuwa yapo makundi ya watu kutoka nchi jirani yameingia nchini kwetu kwa ajili ya kuhakikisha usalama au kwa ajili ya kuzuia maandamano.

Nimelisikia hili wiki mbili kabla ya wiki hii ya uchaguzi, lakini sijasikia tamko lolote likikanusha au kukubali kutoka kwa mamlaka husika.

Kama hili ni kweli inaleta maswali na kama siyo kweli nayo inafikirisha. Kwa nini tufikie hatua ya kusema uongo wa kiasi hiki?

Tunaendelea kuona watu wakilalamika kwa watu kutekwa na kupotezwa. Wanaolalamika wengi wanalishutumu Jeshi la Polisi ambalo nalo linakanusha kuhusika kwa namna yoyote.

Tunajiuliza, iwapo siyo baadhi ya taasisi zetu, basi kama watu hao wanapotea ni nani anafanya hivyo na jeshi linachukua hatua gani?

Inatia shaka pale mtu anapochukuliwa mbele ya umma na polisi, baadaye asionekane kituo chochote cha polisi.

Inakuwaje viongozi watoe matamko ya vitisho kuwataka Watanzania watafute nchi nyingine?



Ni nani asiyetaka kuishi kwa amani na kwa nini?

Waziri wa Mambo ya Ndani amesema wapo watu wanaotoka nje ya nchi wanawafundisha Watanzania utukutu.

Hivi kwa nini Watanzania wafundishwe utukutu?

Tungefika mahali kama nchi tukatafuta kilichotokea nchini. Hivi wale watendaji wa Uhamiaji waliomzuia John Heche kuvuka mpaka kwenda kuzika Kenya nani amewafundisha kufanya hivyo?

Hivi serikali inapomshtaki makamu huyo wa mwenyekiti wa chama cha upinzani, Chadema, na kufungua kesi, ni nani amewafundisha?

Hivi kupotea kwa watu kama Humphrey Polepole aliyekuwa balozi na hadi sasa asionekane katika nchi yenye inteligensia, ni nani aliyeilemaza mifumo ya usalama nchini kiasi hiki?

Huu uchaguzi ulitakiwa uwe kuondoa mgawanyiko kwa watakaopiga kura na watakaoandamana.

Hapo tu panatosha kufanya tutafakari na siyo kwa rais, mgombea wa chama kimojawapo kusema kumuacha akasema kwamba maandamano anayoyategemea ni ya kwenda kupiga kura.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari

# Wafurahia kifungo cha waliotaka kumteka Tarimo



*Mfanyabiashara Deogratias Tarimo*

**Na Mwandishi WETU**

"SASA tumeona haki imetendeka, hili ni jambo zuri sana na hongera kwa vyombo vya serikali kwa kulivalia njuga suala hili hadi mwisho wake."

Hii ni kauli iliyotawala kwenye vinywa vya wakazi wa eneo la Kiluvya, baada ya kutolewa hukumu kwa watu wanne, kati ya sita, wakazi wa Dar es Salaam, walioripotiwa na Pambazuko mwishoni mwa mwaka jana, kwamba walitaka kumteka mkazi wa Kibaha, Deogratias Tarimo (almaarufu Deo Bonge).

Watu hao wamehukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka saba kila mmoja baada ya kupatikana na hatia ya kosa hilo.

Tangu kuanza kuibuka kwa matukio ya utekaji hii ni hukumu ya kwanza kwa watu wanaohusishwa na matukio ya utekaji.

Watuhumiwa hao walihukumiwa wiki iliyopita na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Dar es Salaam, Ramadhan Rugemalila, aliyekuwa akisikiliza shauri lao.

Waliohukumiwa kwenda jela ni askari Fredrick Nsato (21), Isaack Mwaifuani (29) ambaye ni bondia, Benki Mwakalebela (40) na Bato Twelve (32) ambaye naye ni bondia.

Watuhumiwa wawili; Nelson Msela (24) ambaye alikuwa dereva na Anitha Temba (27), waliachiwa huru baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao.

Hakimu Mkazi Mkuu Rugemalila alisema ushahidi ulionyesha washtakiwa hao wanne walijaribu kumteka Tarimo, lakini hawakufanikiwa, hivyo walihukumiwa kwa kosa la kujaribu kumteka mtu.

Mmoja wa majirani waliozungumza na Pambazuko siku chache baada ya jaribio la utekaji huo, juzi aliliambia gazeti hili kuwa hukumu hiyo ni kielelezo cha jinsi serikali inavyofanya kazi.

"Kwa upande wangu nimefurahi kusikia hukumu hiyo imetoka na ninasema haki imetendeka..."

"Kitendo cha watuhumiwa kukamatwa na kufikishwa mahakamani ni kilelezo cha umakini wa vyombo vya dola..."

"Hakika hii ni hatua ya maana sana na endapo haki isingechukuliwa dhidi ya watuhumiwa hawa, wananchi wangeendelea kusema waliohusika ni watu wasiojulikana," alisema jirani huyo kwa sharti la kutotajwa jina.

Tarimo alinusurika kutekwa Novemba 11, mwaka 2024 nje ya Hotel ya Rovvenpec iliyoko Kiluvya, Dar es Salaam, baada ya kuwekewa mtego na mmoja wa watuhumiwa hao.

Katika kuripoti tukio hilo, Pambazuko lilifuatilia sakata hilo kwa kina ambapo waandishi walipiga kambi hotelini hapo na kufanikiwa kupata maelezo ya kina ya tukio zima baada ya picha za video kusambaa mitandaoni zikimuonyesha Tarimo akipambana kujinasua mikononi mwa wanaume waliokuwa wakitaka kumteka.

Inaendelea Uk. 13

# Wafurahia kifungo...

Inatoka Uk. 12

Katika uchunguzi wake, Pambazuko lilibaini kuwa watu hao walikuwa na gari dogo aina ya Toyota Raum lenye namba za usajili T 737 EGE wakati wanafanya tukio hilo.

Miongoni mwa waliozungumzia tukio hilo ni majirani kadhaa wa hoteli hiyo akiwamo mmoja aliyesema kabla ya jaribio la utekaji kutekelezwa majira ya mchana, watekaji hao walifika na gari lao hotelini hapo saa 12 alfajiri ya siku ya tukio kuondoka baada ya muda mfupi.

Alisema ilipotimia majira ya saa nane mchana, watu hao walirudi tena na gari lao na kulipaki nje ya hoteli kabla ya kutaka kumteka Tarimo.

"Walianza kuja saa 12 alfajiri na kuondoka, lakini majira ya saa nane mchana, walirudi tena mpaka hapa kwangu, wakageuza gari lao na kulipaki pale mbele..."

"Wakati naendelea na shughuli zangu hapa, nikasikia watu wanarushiana maneno hapo hotelini, nilipoangalia vizuri nilimuona Bonge amekamatwa, ila anapiga kelele za kuomba msaada," alisema jirani huyo.

Pia, alieleza jinsi mmoja wa wafanyakazi wa hoteli hiyo, alivyokuwa akirekodi video ya tukio hilo akiwa amejibanza jirani na jiko la hoteli yao.

Jirani mwingine alisimulia jinsi watekaji hao walivyopita mara kadhaa na gari lao mbele ya duka lake, saa chache kabla ya utekaji kufanyika.



*Mfanyabiashara Deogratias Tarimo (katikati) akijaribu kujinasua kwenye mikono ya watekaji.*

Habari

# Wahariri wahimiza amani, mwingine akomalia haki



*Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Radio, Joyce Mhavile akizungumza katika mkutano uliowakutanisha wakuu wa vyombo vya habari, wahariri na waandishi kutoka taasisi mbalimbali kuelezea umuhimu wa amani nchini.*

**Na Mwandishi WETU**

BAADHI ya wakuu wa vyombo vya habari na wahariri nchini Tanzania wametoa azimio kuhimiza wananchi kuhakikisha wanalinda amani wakati nchi ikiwa imebakiza siku mbili kufika siku ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

Jumatano ya Oktoba 29, Watanzania wenye sifa na utayari wa kwenda kupiga kura watafanya hivyo kwa kuchagua rais, wabunge, wawakilishi na madiwani.

Wakati wahariri hao wakihimiza amani, mhariri mwingine mwandamizi, Manyerere Jackton, ameshauri mamlaka pia kuhakikisha inatenda na kutunza haki wakati inaposisitizwa amani.

Msimamo wa wahariri hao unaungana na viongozi wa dini na makundi mengine yaliyojitokeza kusisitiza umuhimu wa kutunza amani nchi inapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu unaofanyika keshokutwa, Oktoba 29.

Pamoja na kupongeza wahariri wenzake kwa hatua hiyo, Manyerere ambaye ni mhariri mwandamizi ameandika kwenye mitandao yake ya kijamii kwamba akishauri wahariri na makundi mengine, wakiwamo watawala, kuilea haki; kwani bila haki hakuna amani.

Manyerere amesema kuwa ni vyema kila mtu; bila kujali dhamana yake, akahakikisha amani inatawala, huku haki kwa kila mmoja ikiheshimiwa na kuonekana inalindwa.

Katika azimio lao walilolitoa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wamesema Watanzania - kwa umoja wao, wanatakiwa kukataa kuhudhuria “karamu ya uchochezi” ambayo inaweza kusambaratisha taifa kama ilivyotokea katika mataifa mengine.

“Tanzania imekuwa kisiwa cha amani kwa sababu ya misingi iliyowekwa na waasisi wa taifa letu na utamaduni wa kukaa katika meza ya mazungumzo kumaliza tofauti zetu...”

“Katika siku za karibuni, hapa Tanzania tumesikia kauli zinazochochea chuki na shari, jambo ambalo haliakisi kabisa utamaduni wa Mtanzania...”

“Kauli zinazohamasisha wananchi kufanya vurugu, kuchoma vituo vya mafuta, vituo vya polisi na matukio nyingine, siyo tu ni kosa kisheria, bali ni kauli zisizoakisi umoja wetu na zinazopaswa kukemewa na kila Mtanzania,” walieleza katika tamko lao.

Wahariri hao waliojitambulisha kutoka katika vyombo 11 vikiwemo vya umma, binafsi na taasisi za kihabari, ambavyo ni Shirika la Utandazaji la Zanzibar (ZBC), Azam Media, Tanzania Standards Newspaper (TSN), ITV, Sahara Group, Tanzania Bloggers Network (TBN), Raia Mwema, Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Africa Media Group Ltd (AMGL).

Tamko lao linaeleza kuwa wakuu na wahariri hao wanaamini na kusisitiza kuwa kwenye vurugu, hakuna maelewano na kwamba ni chanzo cha kuvuruga na kuharibu maendeleo.

Wamekemea maneno yenye kuchochea vurugu hasa kipindi hicki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Inaendelea Uk. 15

# Wahariri wahimiza...

Inatoka Uk. 14

Katika tamko hilo, wameainisha pia kuwa mataifa yaliyotumbukia katika machafuko ya kisiasa, vita vya wao kwa wao na mengine kukumbwa na mauaji ya kimbari, yalianza kwa kauli chochezi za mtu mmoja mmoja, baadaye vikundi na hatimaye zikatengeneza "uwendawazimu wa kihalaiki" kupitia vyombo vya habari na mawasiliano ikiwamo mitandao ya kijamii.

**Maoni ya Manyerere**

Muda mfupi baada ya kutolewa kwa azimio hilo, Manyerere Jackton, ambaye ni Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Jamhuri, alitoa maoni yake akieleza kusikitishwa na mwelekeo wa azimio hilo kuwatwisha mzigo wananchi bila kusisitiza pia wajibu wa mamlaka kuhakikisha taifa linakuwa na amani.

Katika ufafanuzi wake, Manyerere alisema wahariri ni mhimili wa nne usio rasmi wa dola, hivyo wanapaswa kuwa kilainishi cha kupunguza msuguano katika mifumo ya kijamii na kisiasa.

"Tutakuwa tunafanya kosa kubwa tukidhani wajibu wa wananchi ni kukubali lolote linalotolewa kwao, ikiwamo wizi wa kura au ghiliba, huku vyombo vya usimamizi wa uchaguzi vikiendelea kuhubiri amani bila haki.



*Mhariri Mwandamizi, Manyerere Jackton*

Amesema suala la bahati mbaya kuwa wahariri, kama makundi mengine, wameingizwa kwenye darasa la kuaminishwa kwamba wenye wajibu wa kulinda amani na utulivu wa taifa ni wanaotawaliwa tu – wapigakura, huku watawala wakishindwa kutetea haki.

Manyerere alieleza kuwa azimio hilo lingepaswa kwenda mbali zaidi, ambapo pamoja na kuwataka wananchi walinde amani, lingenoga kama lingewahimiza watawala na wasimamizi wa vyombo vya utoaji haki kutenda haki.

"Tunakosea mno kuamini kuwa kulinda amani maana yake ni wananchi kukaa kimya hata wanapoona wanadhulumiwa; au haki zao za kuchagua na kuchaguliwa zikivunjwa..."

"Mathalan, tumeshuhudia visa vya mawakala wa baadhi ya vyama kunyimwa viapo, hivyo kukosa sifa ya kushiriki uchaguzi..."

"Tukio kama hilo ndilo lililowahi kusababisha vurugu zilizochukua maisha ya msichana masikini - Akwilina..."

" Tusipokemea dhuluma za aina hii tutakuwa hatutendi haki..."

"Katika mazingira kama haya, azimio lingekuwa lenye usawa kwa pande zote - kuwaasa wananchi walinde amani, lakini pia kuzikumbusha mamlaka za nchi kutenda haki ili kuondoa maung'uniko ya dhuluma ambayo mwisho wake yanaweza kuwa chanzo cha machafuko," alieleza.

Manyerere alibainisha kuwa tamko hilo lingehimiza pia taasisi zote zinazohusika na usimamizi wa uchaguzi - hususan Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), vyama vya siasa, na vyombo vya ulinzi na usalama - kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unazingatia misingi ya haki, uwazi na usawa kwa pande zote.

"Tumekuwa taifa la uchuro na kufoka-foka kwa kigezo cha kulinda amani. Wenye mamlaka watende haki ili wapate sababu za kuwaadhibu barabara hao wanaotaka kuvuruga amani na utulivu wa nchi yetu, amani ya kweli haiwezi kujengwa juu ya udhalimu. Haki ikitendeka, amani hujijenga yenyewe," alisema.

Habari




# Wajaluo bado hawaamini Raila kafariki

Na Mwandishi WETU, aliyekuwa Bondo

BADO kuna vilio, simanzi na maswali mengi juu ya kifo cha aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Kenya, Raila Amolo Odinga.

Jamii ya kabila la Wajaluo walioenea maeneo mengi ya Kenya, kabila ambalo anatoka Raila, wanaendelea kulia, huku wakihoji "mtu wa aina yake anawezaje kufa haraka kiasi hicho?"

Raila ambaye ni maarufu kwa jina la 'Baba' alifariki dunia – kwa ugonjwa wa moyo Oktoba 15, wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Devamatha, iliyoko Koothattukulam, India. Alikuwa na umri wa miaka 80.

Pambazuko ambalo lilifika Nairobi wiki iliyopita na baadaye kuelekea Bondo, Kaunti ya Siaya, limezungumza na watu wengi, ambao wanaendelea kuhoji kifo cha mwanasiasa huyo anayetajwa kupendwa zaidi na Wakenya wa makabila yote.

Katika barabara nyingi za Mji Mkuu wa Kenya, Nairobi, nyimbo za maombolezo zinaendelea kusikika, huku mabango yenye picha za Raila – yaliyoandikwa "Lala Salama Baba" yakionekana kwenye maeneo ya makutano njia kuu za jiji hilo.

Wajaluo kadhaa waliozungumza na Pambazuko Nairobi na Bondo, wanalia kwa sababu wanaamini muda wa Raila kuondoka duniani haukuwa umefika.

"Baba muda wake haukuwa umefika, huenda Mungu alimtuma malaika wake kuchukua mutu mwingine, lakini akakosea na kuchukua Baba, haiwezekani akaenda hivihivi tu, lazima kuna makosa yalitokea," amesema Jonh Owino, dereva wa taksi na mkazi wa Nairobi West, aliyekuwa kiongozi wa safari ya Pambazuko.

Mkazi mwingine wa Bondo, Ouma Aboyo amesema kuwa Raila hakuwa kiongozi wa kufariki muda huu, kwani bado Kenya inamuhitaji kwa kiasi kikubwa kutokana na namna alivyokuwa akipigania taifa, bila kujali ukabila uliogubika nchi hiyo kwa miaka mingi.

"Ahh wacha muchezo bhana, Baba alikuwa mutu ya watu, watu wote walipenda Baba, alikuwa kiungo muhimu sana kwa Kenya yetu, sasa ameondoka sijui itakuwaje, huyu hakuwa mutu ya kawaida, aliibeba Kenya na ndiyo akapendwa zaidi na kila mtu," amesema Ouma, huku akibubujika chozi.

Katika nyumba ya familia ya Odinga, hadi juzi idadi kubwa ya watu walionekana wakiingia na kutoka kwa ajili ya kuhani msiba huo, huku wakifika kutoa heshima kwenye kaburi la Raila, aliyezikwa pembeni mwa baba yake, Jaramogi Oginga Odinga.

Pamoja na kwamba Rais William Ruto alitangaza siku saba za maombolezo, lakini hadi sasa eneo la Bondo, ni kama mwanzo wa msiba.

Bado kuna idadi kubwa ya watu wanaofika na wengine kuweka makazi ya muda kwenye eneo la familia ya Odinga, huku kila siku watu zaidi ya ng'ombe tano zikichinjwa. Inaelezwa ng'ombe hawa wanaletwa na marafiki na ndugu kwa ajili ya kula ili kutimiza mila za Wajaluo kwamba kwenye msiba ni kula, kunywa na kufurahia maisha ya mwenzao.

Haikujulikana lini hasa msiba huo utamalizwa hapo Bondo, kwani wageni wanaendelea kuwasili kila uchao wakiwa wamebeba "zawadi" hasa mifugo kwa ajili ya kitoweo na vinywaji.




*Wanafunzi wa darasa la nne wakiwa darasani*

# Mtaala mpya waanza kutumika darasa la nne

**Na Mwandishi WETU**

TANGU Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 toleo 2023 na mtaala kuboreshwa, kwa mara ya kwanza jumla ya wanafunzi milioni 1.6 wa darasa la nne, wamefanya mtihani wa upimaji wa kitaifa Oktoba 22 na 23 mwaka huu.

Wanafunzi hao wamefanya mitihani ya masomo sita katika michepuo ya sayansi na sanaa.

Chini ya mchepuo wa sayansi masomo yaliyomo ni hisabati, jiografia na mazingira huku sanaa ikihusisha michezo, Kiswahili, Kiingereza na historia ya Tanzania na maadili.

Vilevile kulikuwa na masomo matatu ya lugha ambayo ni Kichina, Kiarabu na Kifaransa.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (Necta), Profesa Said Mohamed, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, kuwa shule 115 za msingi zimejisajili wanafunzi wake kufanya masomo hayo matatu ya lugha.

"Kwa mara ya kwanza kutakuwa na masomo chaguzi matatu ambayo ni lugha ya Kifaransa, Kichina na Kiarabu na katika hili shule 115 zimejisajili, mwanafunzi ana fursa ya kufanya somo moja tu kati ya hayo matatu," amesema.

Profesa Mohamed amesema kati ya shule hizo 115, shule 58 zilijisajili kufanya upimaji huo pamoja na somo chaguzi la Kiarabu lakini pia shule 48 kati ya hizo zimejisajili kufanya somo chaguzi la Kifaransa na shule tisa zimejisajili kufanya somo chaguzi la Kichina.

"Lugha chaguzi zimeongeza idadi ya masomo na kuwa tisa ili kupata kiwango cha ufaulu, tutaangalia masomo aliyofanya vizuri zaidi hata kama ni somo la ziada na tutajumuisha kwenye matokeo," amesema Profesa Mohamed.

Kwa mujibu wa Profesa Mohamed, wanafunzi waliosajiliwa kufanya mitihani hiyo nchi nzima ni 1,582,140 kutoka shule 20,517. Kati yao wasichana ni 817,850 sawa na asilimia 51.69 na wavulana ni 764,290 sawa na asilimia 48.31.

Amesema katika watahiniwa hao waliosajiliwa, wanafunzi 1,485,637 sawa na asilimia 93.27 wanafanya upimaji huo kwa lugha ya Kiswahili huku wanafunzi 106,503 wakitarajiwa kuufanya kwa Kiingereza ambao ni sawa na asilimia 6.73.

"Wapo wanafunzi 5,750 wenye mahitaji maalumu kati yao uoni hafifu ni 1,164; wasioona 111; uziwi 1,161; ulemavu wa akili 1,641 na ulemavu wa viungo 1,673," alisema.

Profesa Mohamed amesema mtihani wa upimaji wa darasa la pili utafanywa kwa siku tatu kuanzia Novemba 18, 19 na 20.

# Tiseza injini ya kukuza uchumi wa Tanzania

**Na Mwandishi WETU**

MAMLAKA ya Uwekezaji na Maeneo Huru ya Kiuchumi (Tiseza), imesema shughuli zake zinalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi kubwa kiuchumi katika eneo la Afrika ifikapo 2030.

Hayo yemeelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tiseza, Gilead Teri, alipokutana na kufanya mazungumzo na wahariri jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

"Uwezekano wa kuyafikia hayo ni mkubwa kwa sababu Tanzania ina kila kitu kinachotakiwa kujenga na kuimarisha uchumi wake," alisisitiza Teri.

Mkurugenzi huyo alisema Tanzania ni nchi ambayo ina vigezo vinavyowezesha kukua na kushamiri kwa uwekezaji na biashara.

Alivitaja baadhi ya vigezo hivyo kuwa ni pamoja na amani, ardhi nzuri, uongozi bora, miundombinu wezeshi na sera bora.

Tiseza ni mamlaka mpya ambayo imeanza kazi Julai mwaka huu baada ya kuunganishwa kilichokuwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Huru ya Kiuchumi (EPZA).

Serikali iliamua kuunganisha taasisi hizo kwa kuwa majukumu yake yalikuwa yanaingiliana na kuunganishwa kwake kumeongeza ufanisi.

Kwa mujibu wa Teri, pamoja na kuunganishwa kwa taasisi hizo, mwaka 2022 serikali pia ilifanya mabadiliko ya sheria ya uwekezaji kwa lengo la kuweka masharti nafuu kwa Watanzania kuwekeza nchini.

Amesema hatua hiyo imeanza kuonyesha mafanikio makubwa kwani katika kipindi cha miaka michache iliyopita idadi ya Watanzania wanaowekeza imekuwa ikiongezeka kwa kasi.


"Lengo ni kuhakikisha kuwa idadi ya Watanzania wanaowekeza inalingana au kuzidi idadi ya wageni wanaowekeza..."

"Hii itawezesha kiasi kikubwa cha mali inayozalishwa kutokana na uwekezaji huo kubaki nchini na kuinufaisha nchi," anasema Teri.

Mwamba wa uwekezaji

Tangu kuanzishwa kwa Tiseza, Tanzania imefungua ukurasa mpya wa usimamizi wa uwekezaji.

Teri anasema taasisi hiyo imewekeza kwenye moja yenye mfumo rahisi, wa kisasa na unaoleta ufanisi, na umeleta mageuzi ambayo yamebadilisha mfumo wa uwekezaji nchini na kupeleka ujumbe wa wazi kwa wawekezaji wa ndani na nje kwamba Tanzania sasa imejipanga vyema kibiashara.




*Mkurugenzi wa Tiseza, Gilead Teri, akiwaonyesha wahariri wa vyombo vya habari chati inayoonyesha kukua kwa idadi ya wawekezaji wazawa katika miaka ya hivi karibuni.*

Ikiwa chini ya Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, Tiseza sasa inafanya kazi kama kituo cha huduma kwa wawekezaji mahali pamoja (OSFC) - mahali ambapo mwekezaji hupata huduma zote muhimu bila kuhangaika na urasimu wa taasisi nyingi.

"Kuanzia usajili wa miradi, utoaji wa leseni hadi vivutio vya kodi, taratibu zote sasa zimeunganishwa na kufanywa kuwa za kidijiti, hivyo kurahisisha uwekezaji kukamilika ndani ya siku saba pekee endapo nyaraka zitakuwa kamili," amesema.

Ufanisi wa Tiseza tayari umeanza kuonekana kupitia kuongezeka kwa idadi ya miradi mipya ya uwekezaji katika sekta muhimu kama viwanda, dawa, kilimo, madini na utalii.

**Wawekezaji wazawa mteremko**

Teri anasema kutokana na kurahisishwa kwa masharti ya uwekezaji kwa wazawa, hivi sasa Tiseza imejikita kuhakikisha kuwa inatoa msukumo wa kuwahudumia Watanzania wenye lengo la kuwekeza nchini.

Anasema mathalan, mtu ambaye anataka kuagiza mitambo ya uzalishaji, Tiseza, kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma, inatoa ushauri wa bure kwa mfanyabiashara kama huyo ili kumrahisishia kutimiza lengo lake hilo.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya wasichana ya Bethsaida ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira magumu iliyopo Mpiji Magoe nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, Raymond Machary akimkabidhi Cheti cha kuhitimu kidato cha nne mwanafunzi Favourest Kivuyo katika Mahafali ya 17 ya Shule hiyo yaliyofanyika hivi karibuni. (NA MPIGA PICHA WETU)*

# Bethsaida walilia ufadhili kusaidia shule

**Na Mwandishi WETU**

UONGOZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bethsaida umewaomba wafadhili kujitokeza kusaidia uendeshaji wa shule hiyo ambayo inahudumia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Akizungumza wakati wa mahafali ya kidato cha nne yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, mkuu wa shule hiyo, Erasto Emmanuel, alisema shule hiyo inategemea zaidi misaada ya wafadhili, lakini idadi yao imepungua kutokana na changamoto za dunia ikiwemo mlipuko wa ugonjwa wa corona na vita kati ya Urusi na Ukraine.

"Kupungua kwa wafadhili kulianza mwaka 2020 kipindi cha corona, na vita kati ya Urusi na Ukraine vimechangia kupunguza zaidi uwezo wao wa kutusaidia," alisema Emmanuel.

Alifafanua kuwa kupungua kwa wafadhili kumesababisha udahili wa wanafunzi kushuka, kwani sasa analazimika kuchukua idadi ndogo ya watoto wanaoweza kuhudumiwa kwa rasilimali zilizopo.

Aidha, alitoa mwito kwa wadau na wafadhili kujitokeza kufadhili watoto mmoja mmoja au kusaidia mahitaji muhimu kama chakula, vifaa vya kujifunzia na mishahara ya walimu ili shule iweze kujiendesha bila wasiwasi.

Mkurugenzi mkuu wa shule hiyo, Raymond Machary, alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma ambapo wanafunzi wengi wanaomaliza wamekuwa wakichaguliwa kuendelea na masomo katika shule mbalimbali za sekondari nchini.

"Mwaka jana wanafunzi wote waliweza kuendelea na masomo, tulikuwa na idadi kubwa ya waliopata division one na two, huku waliopata division three wakiwa saba tu," alisema Machary.

Aliongeza kuwa wanapanga kuendeleza miundombinu ya shule kwa kujenga majengo mapya kutokana na mahitaji makubwa, na kwamba upatikanaji wa wawekezaji utasaidia kufikia lengo hilo.

"Endapo tutapata wawekezaji tutaweza kuongeza majengo na kuwafikia watoto wengi zaidi wanaohitaji msaada wa elimu," aliongeza.

Alisema shule hiyo sasa inaelekeza nguvu zaidi katika mafunzo ya ufundi stadi ili kuwawezesha wanafunzi kujiendeleza na kujitegemea wanapomaliza masomo.

Kwa upande wake, mwanafunzi wa kidato cha nne, Afevest Kivuyo, alitaja changamoto zinazowakabili kuwa ni pamoja na uhaba wa maji safi ya kunywa, chakula na vifaa vya kujifunzia hasa kwa masomo ya sayansi.

"Tunaiomba serikali na wafadhili watusaidie pia kupata fursa za kufanya ziara za kielimu katika maeneo mbalimbali ili kuongeza uelewa wetu," alihitimisha Kivuyo.

# Ahadi za vyama sekta ya ardhi



Na Mwandishi WETU

WIKI hii tunahitimisha dondoo za ilani za vyama vya siasa nchini Tanzania huku zikiwa zimesalia siku mbili taifa kuingia kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kuchagua rais, wabunge, madiwani na wawakilishi.

Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi huo kupitia wagombea wake wamenadi sera na ilani za vyama vyao na kutoa ahadi lukuki kwa lengo la kuwashawishi wapiga kura kuwachagua ili kutawala nchi.

Leo tunaangazia sekta ya ardhi ambayo ndiyo nguzo kuu ya shughuli za kiuchumi na kijamii na kuwa rasilimali ya msingi kwa maendeleo ya nchi.

**AAFP yaeleza umiliki ardhi**

Ilani ya serikali ya Chama cha Wakulima (AAFP), imeahidi kuwa itasimamia haki ya kumiliki ardhi kuwa ya Watanzania tu na haki hiyo italindwa kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi.

Aidha, raia wa kigeni watapewa fursa ya kutumia ardhi kwa ajili ya uwekezaji na maendeleo mengine ya kiuchumi na makazi.

Pamoja na mambo mengine serikali hiyo imeahidi kuwa haki ya kumiliki, kutumia, kuendeleza na kuhifadhi ardhi kwa ajili ya mtu mwingine yeyote au makundi ya kijamii yakiwamo ya wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimbaji madini itazingatiwa.

**NCCR kugawa ardhi isiyoendelezwa**

Chama cha NCCR-Mageuzi, kimeahidi kufanya uhakiki wa mashamba pori yote yasiyoendelezwa kwa kipindi kirefu na kuyagawa upya kwa wananchi kwa kufuata taratibu za kisheria.

Pia, kitaimarisha huduma za utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kuanzisha vyombo vya uamuzi kama vile mahakama ambazo zitahakikisha mashauri ya migogoro ya ardhi yanawasilishwa kwa njia rahisi na kwa gharama nafuu.

**ADA-Tadea kupima ardhi yote**

Sera ya Chama cha African Democratic Alliance (ADA-Tade), imeahidi kuwa endapo kitapata ridhaa ya wananchi kushika dola kitahakikisha ardhi yote inapimwa ili kuondokana na kero ya kuwavunjia nyumba wananchi kwa kigezo cha kupanua barabara.

Katika kuepusha migogoro na migongano isiyokuwa ya lazima ADA-Tadea, kimeahidi kuweka utaratibu wa mipango miji na vijiji kwa kupanga matumizi bora ya ardhi kwa weledi na kwa kipindi cha miaka mia ijayo.

Pia, itagawa kipande cha ardhi kwa kila Mtanzania, kipande hicho kitakuwa mali yake na marufuku kukiuza.

Inaendelea Uk. 21

# Ahadi za vyama...

Inatoka Uk. 20

ADA-Tadea, kimeahidi kuwa hadi kufikia 2030 ni marufuku miji na vijiji kuwa na nyumba za nyasi, isipokuwa zile zinazohusiana na masuala ya utamaduni, maonesho, kimila au matambiko.

Aidha, itarekebisha sheria ya ndoa na talaka ili wanaume na wanawake wapate haki sawa (properyt rights) kulingana na makubaliano.

Endapo kutakuwa na migogoro ya ardhi na mahakama imetupilia mbali mashauri, serikali hiyo itaunda timu maalum ya kitaifa kushughulikia migogoro hiyo.

**ACT Wazalendo kulinda ardhi**

Chama cha ACT Wazalendo, kupitia serikali yake imeahidi kuyashughulikia na kukomesha vitendo vya uporaji wa ardhi, uuzwaji wa mbuga na misitu, mito na maziwa kupigwa mnada, madini, mafuta na gesi kuyaondoa kwenye mikono ya genge la walafi.

ACT Wazalendo imeahidi kuweka ulinzi madhubuti wa ardhi na rasilimali zote za taifa na kuwapa wananchi taarifa sahihi za mikataba ya rasilimali ambazo serikali imewahi kuingia na mikataba yote itakayoingiwa itakuwa ya wazi kwa umma.

**UDP kutoa hati kimila**

Chama cha United Democratic party (UDP), kimewahakikishia wananchi kuwa kikipata ridhaa ya kushika dola, kitatoa hati miliki za kimila au za mtaa kwa wakazi wa maeneo hayo ili waweze kukopa na kujenga upya.

Serikali hiyo imeahidi kushirikiana na sekta binafsi kwa kutumia drone na GIS ili kuharakisha upangaji wa miji na maeneo mapya.

Pia, itapiga marufuku wageni kupewa viwanja bali vitatolewa kwa wazawa waliokwisha omba na kila baada ya miaka mitano serikali hiyo itapitia ripoti za maendeleo ya ardhi.

**CCM kuanzisha benki ya ardhi**

Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa kutambua umuhimu wa ardhi, imeahidi kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji na miji kwa kusajili na kumilikisha hatimiliki.

Itaanzisha benki ya ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya maendeleo na hifadhi.

Imeahidi kuimarisha upatikanaji, utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa huduma na taarifa sahihi za ardhi kwa wakati katika ngazi zote nchini.

Chama hicho kimejinasibu kuwa kitaimarisha miundombinu ya utalii itakayowezesha kufungua vivutio vya utalii na kuvifanya kufikiwa kwa urahisi na usalama.

**Chaumma kufuta kodi**

Ilani ya Chama Cha Ukombozi wa Umma (Chaumma), imeahidi kuipanga ardhi yote, kupima na kumilikisha kisheria kwa hatimiliki sambamba na hilo itawawezesha wananchi wote kuwa na vielelezo vya umiliki ili kuondoa, kudhibiti migogoro ya ardhi.

Chaumma imeahidi kufuta kodi, tozo na ada zote zinazotozwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya uandaaji wa hatimiliki na kuhakikisha hatimiliki zinatolewa bure kwa kila mwananchi mara tu baada ya eneo lake kupimwa.

Ili kumaliza migogoro ya ardhi baina ya wananchi na hifadhi za taifa, serikali ya Chaumma itahakikisha maeneo yote ya hifadhi za taifa yanazungushiwa uzio maalumu utakaowahakikishia wananchi ulinzi na usalama wa kutosha dhidi ya wanyama pori.

Serikali hiyo imeahidi kukomesha rushwa na kupunguza urasimu katika sekta nzima ya usimamizi wa ardhi.

**SAU kugawa ardhi**

Chama cha Sauti ya Umma (SAU), kimeahidi kufanya marekebisho ya ardhi na umiliki kwa kuhakikisha kunakuwapo na ugawaji wa haki wa ardhi na kulinda haki za ardhi za wakulima na kuondosha migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Kushughulikia masuala ya mgawanyo wa ardhi na kukuza mifumo ya kilimo cha ushirika pamoja na kutoa msaada wa kisheria kwa wakulima wanaokabiliwa na migogoro ya ardhi.

Baada ya uchaguzi mkuu tutaendelea kupitia kwa kina ahadi za chama kitakachochaguliwa kuongoza nchi.

# Maofisa Maendeleo ya Jamii waaswa



*Maofisa Maendeleo ya Jamii mkoani Songwe, wakifurahia pikipiki walizopewa na serikali ili kurahisisha majukumu yao.*

**Na Mwandishi WETU, Songwe**

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imekabidhi pikipiki nane kwa Maofisa Maendeleo ya Jamii Songwe, ili kurahisisha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi.

Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika wiki iliyopita, Oktoba 23, 2025 katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka halmashauri nne kati ya tano za mkoa huo.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya pikipiki hizo, naibu katibu mkuu wa wizara hiyo, Felister Mdemu, aliwataka maofisa hao kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujituma zaidi, akisema serikali imewapatia nyenzo hizo muhimu ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao katika jamii.

“Pikipiki hizi ni sehemu ya mikakati ya serikali ya kuwawezesha watumishi kufanya kazi zao kwa ufanisi...”

“Tunatambua mchango mkubwa wa Maofisa Maendeleo ya Jamii katika kufikia wananchi na kuratibu shughuli za maendeleo, hasa katika maeneo ya vijijini,”amesema Mdemu.

Mdemu ameongeza kuwa lengo kuu la kugawa pikipiki hizo ni kutambua thamani ya mchango wa maofisa hao katika jamii, sambamba na kurahisisha kazi za ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, masuala ya ustawi wa jamii, na huduma kwa makundi maalum kama wanawake, vijana, wazee, na watu wenye ulemavu.

“Tunataka kuona matokeo chanya ya uwezeshaji huu. Pikipiki hizi ziwasaidie kufika mbali zaidi, kufuatilia miradi kwa karibu, na kuwahudumia wananchi ipasavyo. Serikali inatarajia mtaongeza uwajibikaji na ubunifu katika kazi zenu,”amesisitiza.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, John Mwaijulu, aliishukuru wizara kwa hatua hiyo, akisema kuwa uwezeshaji huo utasaidia kupunguza changamoto ya usafiri iliyokuwa inawakabili maofisa maendeleo ya jamii kwa muda mrefu.

Tukio kama hilo lilifanyika pia mkoani Iringa ambako katibu mkuu wa wizara hiyo, Dkt. John Jingu, naye alikabidhi pikipiki kwa maofisa maendeleo ya jamii na kuwataka kuzitumia pikipiki hizo kuwafikia wananchi vijijini na kuwahudumia kwa weledi.

“Kwa niaba ya serikali ya Tanzania, nina furaha kukabidhi jumla ya pikipiki kumi kwa maofisa wetu wa Mkoa wa Iringa. Pikipiki hizi ni sehemu ya pikipiki 98 zilizonunuliwa na wizara kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa maofisa katika ngazi ya kata,” amesema Dkt. Jingu.

# Barua za wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Wafagia barabara Dar wamekuwa kero

**Mhariri,**

KUNA hawa wanaofagia barabara maeneo mbalimbali ambao wameajiriwa na manispaa au kampuni, wamekuwa kero hasa kwa sisi tunaosubiri usafiri kwenye vituo vya daladala.

Unakuta umekaa au kusimama, ghafla wanakuja kukutimulia vumbi, ajabu ni kwamba unakuta wafanya usafi hao wanafagia wakati mwingine saa za asubuhi kuelekea mchana.

Unajiuliza asubuhi yote walikuwa wanafanya nini? Nashauri ingependeza wawe wanafagia kuanzia saa 12 hadi saa moja asubuhi, muda ambao abiria siyo wengi vituoni.

**Ezra John,**
**Mbezi,**
**Dar es Salaam.**

## Mitandao ya simu mnatuchosha na meseji

**Mhariri,**

IMEIBUKA tabia ya mitandao ya simu kututumia meseji nyingi kuliko za watu wanaotuhusu kwenye simu zetu.

Siyo mimi tu hata watu wangu wa karibu wamekuwa wakililalamikia hili, maana imekuwa ni kero sasa.

Inatuumiza sana iwe asubuhi, mchana au usiku ni kututumia tu meseji. Sasa basi, wawe wanatulipa maana wamefanya simu zetu kama za biashara. Kiukweli mnatuchosha sana.

Kinachosikitisha ni pale ambapo mtu una shida binafsi, tukiwatafuta kwenye namba ambayo ni 100, mmeweka mlolongo mrefu kuwapata na sauti za roboti.

**Miriam Josephat,**
**Sinza,**
**Dar es Salaam.**

## Matapeli wa ardhi Pwani wadhibitiwe

**Mhariri,**

NI jambo la kawaida kwa wakazi wa Mkoa wa Pwani au nje ya mkoa huo, kununua kipande cha ardhi mkoani humo ambacho tayari kimeshauzwa kwa mtu zaidi ya mmoja.

Vitendo hivi vinafanywa zaidi na matapeli kwa kushirikiana na familia za wenyeji wa mkoa huo pamoja na baadhi ya viongozi wa jamii na serikali wasiokuwa waaminifu.

Aidha, kuna tabia ya baadhi ya familia kutaka kupata fedha za bure kupitia ardhi walizokwishauza zamani wakijifanya hawamtambui mnunuzi mpya.

Isivyokuwa bahati, baadhi ya viongozi wa halmashauri zinazounda mkoa huo wa Pwani, wengine ni wateule wa rais wameingizwa kwenye kushiriki utapeli huo kwa kujua, kutokujua au kwa sababu ya maslahi yao binafsi.

Kupitia gazeti hili la Pambazuko tunawakumbusha viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia sheria na kulinda haki za watu.

**Mwananchi,**
**Halmashauri ya Kibaha Mji,**
**Pwani.**

Wazo Binafsi

# Azimio la wahariri lingesisitiza haki zaidi

Na Manyerere JACKTON

NIMESOMA azimio la wakuu wa vyombo vya habari na wahariri waandamizi Tanzania kuhusu umuhimu wa kutunza amani kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Kwanza, niwapongeze wakuu hao wachache waliothubutu kuchukua dhima ya kuwakilisha vyombo vya habari nchini.

Suala la amani linatuhusu Watanzania wote, na kwa hatua hii, ni jambo la kupongezwa.

Isivyo bahati, sisi wahariri, kama makundi mengine, tumeingizwa kwenye darasa la kuaminishwa kwamba wenye wajibu wa kulinda amani na utulivu wa taifa ni wanaotawaliwa tu; wapigakura.

Matamko ya wanasiasa, viongozi wa dini, wagombea, wapambe wa vyama, polisi na viongozi wa vyombo vya utoaji haki, mara nyingi huonyesha kana kwamba jukumu la kulinda amani ni la wananchi pekee.

Azimio la wakuu wa vyombo vya habari lingepaswa kwenda mbali zaidi na kunoga kama lingewahimiza watawala na wasimamizi wa vyombo vya utoaji haki kutenda haki kwa wapigakura na wagombea wote, ili kuondoa malalamiko yanayosababisha uvunjifu wa amani.

Tunakosea mno kuamini kuwa kulinda amani maana yake ni wananchi kukaa kimya hata wanapoona wanadhulumiwa; au haki zao za kuchagua na kuchaguliwa zikivunjwa.

Mathalan, tumeshuhudia visa vya mawakala wa baadhi ya vyama kunyimwa viapo, hivyo kukosa sifa ya kushiriki uchaguzi.

Tukio kama hilo ndilo lililowahi kusababisha vurugu zilizochukua maisha ya msichana masikini — Akwilina. Tusipokemea dhuluma za aina hii tutakuwa hatutendi haki.

Katika mazingira kama haya, azimio lingekuwa na mizania ya usawa kwa pande zote; kuwaasa wananchi walinde amani, lakini pia kuzikumbusha mamlaka za nchi kutenda haki ili kuondoa maung'uniko ya dhuluma ambayo mwisho wake yanaweza kuwa chanzo cha machafuko.

Ingependeza iwapo ndani ya tamko hilo kungewekwa maneno ya aina hii; "Tunazihimiza taasisi zote zinazohusika na usimamizi wa uchaguzi — hususan Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), vyama vya siasa, na vyombo vya ulinzi na usalama, kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unazingatia misingi ya haki, uwazi na usawa kwa pande zote."

Bila kuweka msisitizo huo, tafsiri inayobaki ni kwamba wapigakura wanapaswa kukaa kimya hata wanapoibiwa kura, kwa kisingizio cha kulinda amani ya nchi.

Ndiyo maana sasa wakuu wa wilaya, mikoa, mawaziri, polisi, na watawala wote wanawafokea hao wanaodhaniwa wanataka kuvunja amani.

Tumekuwa taifa la uchuro na kufoka-foka kwa kigezo cha kulinda amani. Wenye mamlaka watende haki ili wapate sababu za kuwaadhibu barabara hao wanaotaka kuvuruga amani na utulivu wa nchi yetu.

Sisi wahariri ni mhimili wa nne usio rasmi wa dola. Tunapaswa kuwa kilainishi kupunguza msuguano katika mifumo ya kijamii na kisiasa.

Tutakuwa tunafanya kosa kubwa tukidhani wajibu wa wananchi ni kukubali lolote linalotolewa kwao, ikiwamo wizi wa kura au ghiliba, huku vyombo vya usimamizi wa uchaguzi vikiendelea kuhubiri amani bila haki.

Amani ya kweli haiwezi kujengwa juu ya udhalimu.

***Haki ikitendeka, amani hujijenga yenyewe.***

***Mwandishi ni Naibu Mhariri wa Gazeti la Jamhuri.***

# Serikali yashtushwa taarifa ya Amnesty

**Na Mwandishi WETU**

> **Mahakama inaendelea kuwa huru na kila mtu ana haki ya kupata usikilizwaji wa haki kwa mujibu wa sheria za ndani na za kimataifa".**

SERIKALI ya Tanzania imeijibu Shirika la Amnesty International, kuhusu taarifa iliyoitoa ikizishutumu mamlaka zake kwa madai ya kukiuka haki za binadamu na ukandamizaji watu kuelekea Uchaguzi Mkuu, 2025.

Kupitia taarifa iliyotolewa juzi Oktoba 25,2025 na Msemaji Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Gerson Msigwa, ilieleza masikitiko yake na madai hayo ya Amnesty aliyosema hayana uthibitisho.

Taarifa hiyo ya Msigwa ilieleza kuwa serikali haikupewa fursa na haki ya kujibu kabla ya kuchapishwa taarifa hiyo ya Amnesty.

Wakati taarifa hiyo ya serikali ikisema hivyo, Amnesty katika taarifa yake ilibainisha kuwa mamlaka za Tanzania hazikujibu ombi lao la kutoa maoni.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea kwa masikitiko taarifa fupi iliyotolewa na Amnesty na imeonyesha wasiwasi mkubwa juu ya maudhui na mtazamo wa madai yaliyomo ndani yake," amesema Msigwa.

Msemaji huyo wa serikali alifafanua kuwa dhamira ya serikali ni kulinda na kuelendeleza haki za binadamu kama ilivyohakikishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (na marekebisho yake).

"Pia, Tanzania inazingatia katika mikataba ya kimataifa na ya kikanda ambayo Tanzania imeridhia, ikiwemo ICCPR, mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Mkataba Dhidi ya Mateso,"amesema Msigwa.

Msigwa alilaani taarifa hiyo ya Amnesty akisema mtindo wake unadhoofisha misingi ya uhalisia na kuheshimiana ambayo inapaswa kuongoza mazungumzo kuhusu haki za binadamu kimataifa.

"Maelezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo yanaonyesha kwamba kukamatwa kiholela, kupotezwa kwa watu kwa kulazimishwa na kukandamiza uhuru wa raia, hayana uhusiano wowote na uhalisia wa kisheria na wa taasisi zilizopo nchini…"

"Tanzania inatekeleza sera ya kutovumilia kabisa mateso au aina yoyote ya adhabu ya kikatili na isiyo ya kibinadamu. Madai ya aina hiyo huchunguzwa na mamlaka husika," alisema Msigwa.

Katika taarifa hiyo, Msigwa amesisitiza kuwa uhuru wa kujieleza, kukusanyika kwa amani na upatikanaji wa taarifa vinalindwa na Katiba.

"Serikali ya Tanzania haitetei vitendo vya kupotezwa kwa watu wala mauaji. Kila tukio linaloripotiwa hufanyiwa uchunguzi wa kina na kuchukuliwa hatua za kisheria…"

"Mahakama inaendelea kuwa huru na kila mtu ana haki ya kupata usikilizwaji wa haki kwa mujibu wa sheria za ndani na za kimataifa".

Kuhusu mchakato wa uchaguzi, Msigwa amesema Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) inafanya kazi kwa uhuru kama ilivyohakikishwa na Kifungu cha 74 (11) cha Katiba.

**Taarifa ya Amnesty**

Oktoba 20, 2025, Amnesty ilitoa taarifa yake yenye kichwa cha habari "Unopposed, Unchecked, Unjust: 'Wave of Terror' Sweeps Tanzania Ahead of 2025 Vote".

Taarifa hiyo ya Amnesty ilieleza kuwa mamlaka za Tanzania zimeongeza ukandamizaji dhidi ya wapinzani wa kisiasa, waandishi wa habari, asasi za kiraia na watetezi wa haki za binadamu kwa lengo la kuwapa hofu.

Katika tarifa hiyo shirika hilo, inaeleza kuwa kabla ya kuandaa taarifa hiyo iliwahoji watu 43 wakiwemo waathirika, mashahidi, ndugu wa waathirika, wawakilishi wa kisheria na wanachama wa asasi za kiraia na pia kukusanya taarifa za mashambulizi kutoka vyombo vya habari.

Kimataifa

# Tinubu apangua makamanda wa jeshi

RAIS wa Nigeria, Bola Ahmed Tinubu, amefanya mabadiliko makubwa katika safu za juu za uongozi wa kijeshi.

Uamuzi huo unaeleza kuwa ni sehemu ya jitihada zake kuimarisha usalama wa taifa linalokabiliwa na changamoto za muda mrefu za kiusalama.

Ofisi ya Rais – Ikulu, ilitangaza uteuzi huo Ijumaa, ikieleza kuwa utekelezaji utaanza mara moja.

Katika mabadiliko hayo, Jenerali Olufemi Oluyede ameteuliwa kuwa Kamanda Mkuu wa Ulinzi, akichukua nafasi ya Jenerali Christopher Musa, ambaye alihudumu tangu mwanzoni mwa utawala wa Tinubu.

Uteuzi huu unakuja wakati taifa hilo likiwa bado linapambana na vitisho vinavyotoka kwa makundi ya wanamgambo wa Boko Haram na Islamic State West Africa Province (ISWAP) katika maeneo ya kaskazini-mashariki mwa Nigeria.


> **“Serikali imejizatiti kuona kuwa usalama wa raia unakuwa kipaumbele cha kitaifa,” ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo kutoka Ofisi ya Rais.**

Katika mabadiliko hayo, Meja Jenerali Waidi Shaibu amechukua nafasi ya juu ya kuwa mkuu wa vikosi vyote, huku Sunday Aneke akiteuliwa kuwa Kiongozi wa Jeshi la Anga, na Rear Admiral  Abbas akiongoza Jeshi la Majini.

Mabadiliko haya yanaonekana kama juhudi za Rais Tinubu kuleta damu mpya yenye mitazamo tofauti katika sekta ya ulinzi, ili kuongeza ufanisi na weledi wa vikosi vya jeshi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu ya Abuja, Meja Jenerali Emmanuel Undiendeye ataendelea kushikilia nafasi yake kama Kiongozi wa Upelelezi wa Ulinzi, nafasi muhimu inayohusisha ukusanyaji wa taarifa za kiusalama na uratibu wa operesheni nyeti za kijeshi nchini humo.

Nigeria, taifa lenye idadi ya watu zaidi ya milioni 200, limekuwa likikabiliwa na changamoto nyingi za kiusalama, kutoka ugaidi wa wanamgambo wa kaskazini-mashariki, uharamia katika Delta ya Niger, hadi mizozo ya wakulima na wafugaji katika maeneo ya kati mwa nchi hiyo.



*Rais wa Nigeria, Bola Tinubu*

Wachambuzi wa masuala ya usalama wanasema kuwa mabadiliko haya ni ishara ya jitihada za Rais Tinubu kurejesha imani kwa jeshi na wananchi wake.

“Serikali imejizatiti kuona kuwa usalama wa raia unakuwa kipaumbele cha kitaifa,” ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo kutoka Ofisi ya Rais.


Kwa sasa, macho ya wengi yameelekezwa kwa viongozi wapya wa jeshi kuona iwapo watafanikiwa kurejesha amani katika taifa ambalo limekuwa likihangaika kwa muda mrefu na mashambulizi ya kigaidi, uporaji, na utekaji nyara unaolenga raia wasio na hatia.



Na Rashid MTAGALUKA



# Tanzania machoni pa dunia



UCHAGUZI Mkuu wa Tanzania unafanyika keshokutwa; Oktoba 29, 2025, na hadi sasa umeiweka Tanzania katika macho ya dunia ikitambuliwa kuwa na ngome ya utulivu wa kisiasa na majaribio ya kidemokrasia Afrika.

Siku chache zilizopita, wageni kutoka pande mbalimbali za dunia, wameanza kuwasili nchini wakiwamo waangalizi wa Umoja wa Afrika (AU), Jumuia ya Madola, Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na taasisi za kimataifa za uchaguzi.

Hawa wanakuja kushuhudia yanayoendelea kujiri kwenye maandalizi kabla ya siku ya kupiga kura.

Uwepo wao unaashiria imani kubwa kuwa Tanzania, licha ya changamoto za kisiasa zilizowahi kujitokeza, bado ni kitovu cha amani na mafunzo kwa mataifa mengine ya Afrika yanayojitahidi kuimarisha taasisi za kidemokrasia.

Kwa mujibu wa taarifa za awali kutoka baadhi ya timu za waangalizi, mazingira ya maandalizi ya uchaguzi yameonyesha ufanisi mkubwa wa Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) katika kuhakikisha uwazi na ushiriki mpana wa wadau.

Vyama vya siasa vimepata nafasi ya kufanya kampeni kwa amani, vyombo vya habari vimeendelea kuripoti kwa uwiano, na vyombo vya ulinzi vimeahidi kulinda haki ya kila raia kupiga kura bila hofu.

Dunia inaona hatua hii ni mwendelezo wa Tanzania kuimarisha misingi ya utawala bora na kuheshimu sauti ya wananchi wake.

Kwa miongo kadhaa, Tanzania imejijengea heshima ya kuwa mfano wa utulivu katika bara lililokumbwa na migogoro mingi ya kisiasa.

Siri ya mafanikio haya iko katika urithi wa umoja wa kitaifa uliosimikwa tangu enzi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Mfumo wa kisiasa wa nchi hii, umekuwa ukitilia mkazo zaidi mazungumzo na maridhiano kuliko migongano, jambo linaloifanya Tanzania kuwa kivutio cha kimataifa katika ujenzi wa demokrasia endelevu.

Aidha, dunia inaitazama Tanzania kuwa ni kielelezo cha mabadiliko chanya chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye alifungua ukurasa mpya wa majadiliano na wadau wa siasa, mashirika ya kiraia, na vyombo vya habari.

Hatua hizo zimeleta upepo mpya wa matumaini na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na mataifa mengine, hasa yale ya magharibi yaliyokuwa na wasiwasi kuhusu uhuru wa kisiasa miaka michache iliyopita.

Kwa ujumla, uchaguzi huu umegeuka kipimo cha uhalisia wa demokrasia ya Tanzania na uthibitisho kwamba nchi hii inaendelea kuamini katika nguvu ya kura, mazungumzo na umoja wa kitaifa.

Kwamba hivi sasa dunia inashuhudia taifa linalojifunza, kubadilika na kujijenga upya katika njia ya amani ikiibua taswira mpya kwamba Tanzania siyo tu kivutio cha utalii, bali pia taa ya demokrasia Afrika.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

# Habari katika Picha

*Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mjumbe Maalum na Waziri wa Ushirikiano wa Kikanda wa nchi hiyo, Floribert Anzuluni aliye-wasilisha ujumbe maalum wa Rais wa Congo (DRC), Felix Antoine Tshisekedi, baada ya kuupokea, Ikulu jijini Dar es Salaam, mwis-honi mwa wiki. (Picha na Ikulu).*






*Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Augustino Senga (kushoto), akimkabidhi magari mawili mapya aina ya Robur Armored TLC300, Mkuu wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia Mkoa wa Son-gwe, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Sija Kadogosa mwishoni mwa wiki. (Picha na Issa Mwadangala).*



*Wajasiriamali wakisubiri wateja wa ndizi katika eneo la Mto wa Mbu wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)*


*Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dkt. Asha-rose Migiro wakifu-rahia jambo katika mku-tano wa kampeni katika majimbo ya Mbagala, Kigamboni, Chamazi na Temeke uliofanyika uwan-ja wa TANESCO, Buza jijini Dar es Salaam, mwisho-ni mwa wiki. (Picha na Ikulu).*



# Jinsi ya kusoma Pambazuko



## Uhusiano



Na Anti MSHAURI







# Wanandoa zingatieni haya

HABARI za leo msomaji wangu wa safu ya uhusiano.

Wiki hii nitazungumzia umuhimu wa wanandoa kulinda ndoa zao.

Uhusiano wa mume na mke unajengwa kwa misingi ya kuheshimiana na kusikilizana na misingi hiyo ndiyo inayoweza kuwawezesha kuishi kwa amani na furaha.

Mwanaume ndiye kichwa cha familia, hivyo katika maisha hayo, anapaswa kuhakikisha anaihudumia familia yake kwa hali na mali kwa kuipatia mahitaji muhimu ingawa haikatazwi mke kuisaidia familia.

Wakati wote wa maisha ya wawili hao, mwanamke anapaswa kuwa mtiifu kwa mumewe; kama ana shughuli za kumwingizia kipato iwe kuajiriwa au kujiajiri anatakiwa kuhakikisha nyumbani kwake hakuna dosari yoyote.

Mwanamke hakikisha unampatia mumeo haki zote za ndani hasa ya ndoa, kuhakikisha anakula chakula kilichoandaliwa vizuri (hapa unashauriwa umwandalie mwenyewe kadiri inavyowezekana).

Mke unatakiwa kuwa mtiifu kwa mumewe katika yote yanayopaswa; wanawake wengi wamekuwa wakishindwa kuwatii waume zao na kujiamulia mambo bila kuwashirikisha jambo ambalo halileti picha nzuri, wengine hasa wanaowazidi vipato waume zao wamekuwa viburi.

Wanandoa eleweni kwamba ndoa haijengwi na pesa, mali au maisha ya kutoelewana bali masikilizano kati yenu. Kiburi na kutomtii mume kunaweza kusababisha mafarakano.

Vivyo hivyo, kwa mume anapaswa kumuheshimu mkewe na kumuona wa muhimu katika maisha kwani heshima ndiyo nguzo ambayo inaweza kuifanya nyumba yenu kuwa imara zaidi.

Kuna baadhi ya wanaume ambao wamekuwa wakiwaonyesha wake zao vitendo vinavyowaumiza na kuwasababishia maumivu.

Miongoni mwa matendo hayo ni kuvunja uaminifu na kuanzisha mahusiano nje ya ndoa hali inayowavunja moyo wake zao. Tabia hii imekuwa ikikomaa siku hadi siku na kusababisha ndoa nyingi kuvunjika.

Ili kudhihiti hali hiyo wanandoa wanapaswa kuheshimu maagano yao ya ndoa na kuachana na mambo mengine ya dunia yasiyofaa.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***



# Aina za pochi zinazobamba mwaka 2025



KILA mwaka huwa kuna aina mpya za pochi za wanawake zenye mitindo, rangi na miundo tofauti kulingana na mwelekeo wa 'fashion trends' wa dunia nzima.

Ifuatayo ni aina za pochi za wanawake zinazoendelea kubamba kwa mwaka huu wa 2025;

**Pochi ya tote (tote bag)**

*Ina muundo mpana, inaweza kubeba vitu vingi ikiwemo; laptop, kitabu na vazi la ziada.

*Hii inafaa zaidi kwa safari au kazini kama unabeba laptop.

**Pochi ya crossbody**

*Ni ndogo lakini ina kazi nyingi; inafaa zaidi kwa matembezi ya mchana, kwa safari, shopping au hata mtoko wa usiku.

**Pochi ya Hobo (Hobo Bag)**

*Muundo wake umepanuka kidogo na ni imara sana.

*Inafaa kwa kubeba kazini na mtoko wa kawaida. Ikiwa unapenda pochi rahisi basi hobo ni chaguo sahihi zaidi.

**Shoulder bag**

*Hii mikono au mikanda yake ni ya juu, imekaa kizamani lakini imeboreshwa zaidi kwa mwaka huu 2025.

*Inafaa kubeba kazini na kwenye matukio mengine ya kawaida.

# Ondoa weusi kwapani kwa nyanya, sukari


WEUSI kwapani unasumbua watu wengi, wanaume kwa wanawake, hapa nimekuwekea namna bora ya kukabiliana na tatizo hilo kwa kutumia nyanya na sukari.

Dondoo

Chukua nyanya ikate kati kisha weka sukari juu yake na kisha sugulia eneo ambalo lina weusi.

Fanya hivi mara mbili hadi tatu kwa wiki kwa matokeo mazuri zaidi.







# Bob Junior amwangukia Rais Samia

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Bongo Fleva, Raheem Rummy - almaarufu Bob Junior, ameomba msaada wa kifedha kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ili aweze kwenda India kupata matibabu.

Bob Junior, ambaye amekuwa akikabiliwa na matatizo ya kiafya kwa muda mrefu, ameandika ujumbe huo kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Salaam aleykum mama, mimi ni msanii wa kizazi kipya. Napitia changamoto ngumu sana ya kuumwa jicho ambalo limefanyiwa upasuaji, lakini sijapona, pamoja na maradhi ya moyo…"

"Natakiwa kwenda India kutibiwa, lakini hali yangu kiuchumi siyo nzuri kabisa. Naomba msaada kwako mama, Allah akubariki sana," ameandika msanii huyo.

Amesema matatizo yake ya kiafya yamemfanya kushindwa kuendelea na shughuli zake za muziki, jambo ambalo limeathiri maisha yake.


# Kanye achukizwa Kim anavyomlea binti yao

Na Mwandishi WETU


NORTH, binti wa Kim Kardashian na Kanye West mwenye umri wa miaka 12, ameteka mitandao ya kijamii kutokana na namna anavyojiweka kama mtu mzima.

Binti huyo anaonekana kufuata mfano wa mama yake, Kim baada ya kuonekana na tatoo za bandia usoni, nywele zenye rangi ya bluu, lensi za macho ya bluu, huku mikono akipamba kwa hena.

Kutokana na hilo, baba yake hakufurahishwa na mabadiliko hayo, huku akionyesha wasiwasi wake kwa Kim jinsi anavyomlea binti yao.



Michezo Kimataifa



Nahodha wa Liverpool, Virgil van Dijk akiwa ameshika kichwa baada ya kupoteza mchezo wao dhidi ya Brentford kwa mabao 3-2 juzi.

# Bundi aendelea kukalia ndoto Liverpool



Kocha wa Liverpool, Arne Slot

Na Mwandishi WETU

MAJOGOO wa Jiji la Liverpool, Uingereza ni wazi mambo yanazidi kuwaendea mrama siku hadi siku baada ya kipigo cha nne mfululizo katika Ligi Kuu ya England.

Liverpool ambaye aliteremka dimbani kumenyana na Brentford mwishoni mwa wiki, ilijikuta ikipokea kipigo kizito cha magoli 3-2 usiku wa Jumamosi katika Uwanja wa Gtech Community jijini London.

Liverpool imepoteza mechi ya tano katika michuano yote, yaani katika mechi sita za mwisho ilizocheza mfululizo, imeshinda moja tu ugenini dhidi ya Frankfurt ya Ujerumani.

Huku akipokea kichapo kutoka kwa Cystal Palace 2-1, Manchester United 2-1, Chelsea 2-1, Galatasaray ya Uturuki 1-0 na sasa Brentford.

Mabao ya Brentford yalifungwa na Dango Ouattara dakika ya 5, Kevin Schade dakika ya 45 kipindi cha kwanza pamoja na mshambuliaji Igor Thiago dakika ya 60.

Mabao ya Liverpool yalifungwa na mshambuliaji nyota Mohamed Salah dakika ya lala salama 89, pamoja na beki wa kushoto Milos Kerkez dakika ya nyongeza kipindi cha kwanza.

Kocha Arne Slot ana kibarua kigumu zaidi kwani ameanza kuliona joto la Ligi Kuu ya England ya kuwa kila mechi ni 'big match' kwelikweli.

Wachambuzi wengi wameendelea kumkosoa kocha huyo na kusema ametumia pesa nyingi kwenye usajili kwa kuboresha eneo la ushambuliaji zaidi na kusahau eneo muhimu la ulinzi.

Liverpool inaelezwa kutokuwa na kiungo wa ulinzi mwenye maarifa na msuli wa kutosha.

Kila shabiki wa Liverpool ameanza kupoteza matumaini na ubingwa wa ligi na swali ambalo wanajiuliza kuwa watajinasuaje hapa au ndio vipigo vitaendelea kuwaandama?

Pambazuko

MICHEZO

Jumatatu, Oktoba 27-Novemba 2,2025





# Timu za Tanzania zaandika historia




*Pacome Zouzoua*

Na Mwandishi WETU

HATIMAYE historia imeandikwa kwa wino wa dhahabu na itachukua muda mrefu kufutika vizazi na vizazi vitashuhudia timu nne za Tanzania kwa mara ya kwanza kutinga hatua ya makundi michuano ya Klabu Bingwa pamoja na Shirikisho Afrika.

Vilabu hivyo ni Azam FC, Simba SC, Yanga SC pamoja na Singida Black Stars. Azam ndio ilikuwa timu ya kwanza kutinga hatua ya makundi kwa kuibugiza klabu ya KMKM ya Zanzibar magoli 7-0, mechi ya mkondo wa pili iliyopigwa katika Uwanja wa Chamazi Complex, Dar es Salaam.

**Yanga nayo yatinga kibabe**

Ni wazi kuwa 'Wananchi' wa Jangwani, Yanga wameonesha ukomavu wa hali ya juu kwa kutinga hatua ya makundi kwa kuicharaza Silver Strikers mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Magoli ya Yanga yalifungwa na nahodha Dickson Job dakika ya tano na bao la pili liliwekwa kimiani na kiungo-bamia, Pacome Zouzoua dakika ya 33 kipindi cha kwanza.

Wakati huohuo, Klabu ya Yanga imemtambulisha Pedro Goncalves raia wa Ureno kuwa kocha mkuu wa timu hiyo akichukua mikoba ya Romain Folz aliyefurushwa hivi karibuni. Pedro amewahi kufundisha Timu ya Sporting CP ya Ureno, De Agosto ya Angola pamoja na Timu ya Taifa ya Angola.

**Singida waandika historia**

Klabu ya Singida Black Stars imetinga hatua ya makundi ya kombe la Shirikisho Afrika (CAFCC) kwa mara ya kwanza kihistoria kufuatia ushindi wa jumla wa mafoli 4-2 dhidi ya Flambeau du Centre ya Burundi kwenye hatua ya pili.

**Simba hiyoo makundi**

Mnyama naye hakuwa nyuma katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika (CAFCL) kwenye mchezo wao dhidi ya Nsingizini Hotspurs ya Eswatini ulimalizika kwa sare ya bila kufungana (0-0) lakini Simba ilisonga mbele.

Sasa ni rasmi vilabu vyote vinne vimetinga hatua ya makundi kwenye michuano ya kimataifa ya CAF, sisi Pambazuko tunawatakia kila la kheri wawakilishi wetu.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION